

* MTANZANIA UK 18
TADB yawakopesha Sh mil 200 wavuvi *Na MWANDISHI WETU
-UKEREWE

CHAMA cha Ushirika cha Wavuvi Bukasiga kilichopo wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, kimekabidhiwa mkopo wa Sh milioni 200 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Fedha hizo ni kwa ujenzi wa kiwanda cha barafu na kujenga mtambo wa kukaushia dagaa ili kuongeza thamani ya samaki na mazao yake.

Akizungumza wakati akikabidhi hundi ya fedha hizo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema ili kufikia azma hiyo lazima wavuvi wachape kazi kwa nguvu kwa sababu hakuna njia ya mkato ya kufikia maendeleo.

Alisema Serikali kipindi cha awamu ya kwanza, imeweka mikakati mizuri na kuthubutu kuhakikisha wavuvi wanaanza kuaminiwa na kukopesha kupitia TADB na kufanua kuwa Rais DK John Magufuli ameweka mazingira ya kufanya wavuvi waaminike na taasisi za fedha na kupeua mikopo ili kujimarisha katika shughuli zao.

"Hii benki tangu ianze ina miaka mitano sasa, imewakopesha

Watanzania katika nyanja za kilimo, mifugo na uvuvi zaidi ya shilingi bilioni 170, tangu uhai wa taifa, wavuvi wameanza kuaminiwa na kukopesha.

"Samaki siyo zao la msimu, ni la mwaka mzima, wakati ndiyo huu wa kutimiza lengo la rais la kuwa na viwanda vidogo vitakavyoleta tija na maendeleo kwa wananchi na kukuza uchumi wa nchi," alisema Ulega.

Aliwataka kuwa wazalendo, waadilifu katika kusimamia vyema fedha walizopata, huku akitaka Taasisi ya Kuzua na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani humo kuwashauri wanachama mapema kuliko kusubiri hadi waharibikiwe.

Pia alito onyo kwa watendaji kutotegemea posho katika kutimiza majukumu.

"Mkakati wa Serikali ni kuunda vyama vya ushirika vya wafugaji na wavuvi, upande wa wavuvi takwimu zipo vizuri. Endapo mkirudisha mikopo yenu vizuri, nitakuwa wakili wenu ambaye nitamweleza mkurugenzi wa TADB awaongeze mkopo," alisema Ulega.

Mkurugenzi Mkuu wa TADB, Japhet Justine, alisema uvuvi ni eneo muhimu Ziwa Victoria, kwani

samaki wanapatikana kwa wingi, kinachohitajika ni kufanya uvuvi wa kisasa ili kubadilisha rasilimali kuwa fursa na maono ya rais kuwa vitendo.

Justine alisema wameweza kutekeleza upatikanaji wa mikopo huo baada ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuweka mikakati ya kuhakikisha inatekeleza uvuvi uwe wa kisasa utakaonyesha fursa zaidi.

"Sisi tunataka kiwanda cha barafu, mashine au kifaa cha kuanika dagaa ambao wanaweza kudumu hadi mwaka mmoja wakiwa vizuri.

"Tunafanya haya ili rasilimali zetu ziwe kwenye tija, hizi ni nyakati za ushindani, ubora wa bidhaa ni muhimu. tupo pamoja nanyi na hatutawatupa sisi kama benki ya kilimo," alisema Justine.

Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi Bukasiga, Erasto Majula, alisema wanachama waliopo katika ushirika huo ni 62 na wana viwanja vitatu ambavyo hutumika kwa uendeshaji wa shughuli za uvuvi.

Alisema kiwanja kimoja chenye ukubwa wa takribani ekari moja watajenga kiwanda cha barafu, kiwanja kingine wanatarajia kujenga mtambo wa kukaushia dagaa huku kingine kikiwa kimejengwa ofisi na banda la vyumba 22 kwa ajili ya kambi ya

wavuvi.

Majula alisema lengo lao ni kuendesha shughuli za uvuvi endelevu katika eneo la Kata ya Ilangala na Kakukuru, pamoja na kusimamia masilahi ya wavuvi kwa njia ya uwakilishi katika mikutano ya wadau na Serikali.

"Hivyo tulikubaliana kutafuta mtaji wa kuimarisha shughuli zetu kwa lengo la kuongeza kipato ngazi ya kaya na kuchangia katika pato la taifa," alisema Majula.

Akizungumza baada ya kupokea hundi, mmoja wa wanufaika wa fedha hizo, Jumbula Lugola alitoa shukrani kwa waziri huyo kwa kuwahamisha na kwamba mwanzo wallichukulia suala hilo kama hadithi, lakini wameanza kuona matokeo yake.

Alisema kuwa wataenda kutekeleza vyema yale wananotakiwa kufanya hasa ujenzi wa kiwanda cha barafu.

MGAWO

HaloPesa kugawa Sh bilioni moja kwa wateja

Na MWANDISHI WETU
-DAR ES SALAAM

KATIKA mwendelezo wa kutoa huduma bora za kifedha nchini, Kampuni ya mawasiliano ya simu ya Halotel kupitia huduma zake za kifedha za HaloPesa, inatarajia kufanya gawio kwa wateja wake.

Hatua hiyo ni ya kwanza kwa HaloPesa kutoa gawio Sh bilioni moja kwa wateja wake zaidi ya milioni 19 ambao ni pamoja na wateja binafsi, mawakala na washirika wake mbalimbali wanaotumia huduma za HaloPesa.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha HaloPesa, Magea Wandwi, alisema wateja wao watapatiwa gawio hilo kupitia akaunti zao za HaloPesa.

"Wateja watapata sehemu ya gawio hili linalotokana na faida iliyozalishwa kutoka akaunti za HaloPesa Trust zilizoko katika benki mbalimbali kati ya Oktoba 2016 na Desemba 2018," alisema Wandwi.

Alisema faida hiyo ni haki ya wateja na hivyo HaloPesa ina shauku na furaha kubwa ya kuwalipa wateja wetu gawio hilo kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali tokeni Kuu ya Tanzania (BoT).

"Gawio hilo ni la kwanza kwa wateja wetu, na litatolewa ndani ya mwezi mmoja toka sasa.

"Kiasi cha gawio ambacho mteja wa HaloPesa atakipata anaweza kutumia atakavyo, ikiwa ni pamoja na kutoa au kufanya miamala mbalimbali," alisema Wandwi.



- Picha: MPIGAPICHA WETU

MSAADA: Naibu Waziri wa Kilimo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine (wa tano kulia), wakiwa wameshika mfano wa hundi ya Sh milioni 200 waliyokabidhi kwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Wavuvi Bukasiga, Kijiji cha Katuturu wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, Jumbura Lugola (wa tatu kulia) iliyoitolewa na TADB.

Wafanyabiashara vifaa vya ujenzi waaswa kutopunja wateja

Na MWANDISHI WETU
-DAR ES SALAAM

WAKALA wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Kinondoni, umewaasa wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi kutumia vipimo sahihi vilivyohakikiwa na wakala huo kuepuka kupunja wateja.

Akizungumza juzi wakati wa ukaguzi katika maduka ya vifaa vya ujenzi yaliyopo Mwenge, Kaimu Meneja Wakala Vipimo Mkoa wa Kinondoni, Charles Mavunde, alisema ukaguzi wa kushtuka ulilenga kuangalia matumizi sahihi ya vipimo katika kuwahudumia wateja.

"Sekta ya ujenzi ni muhimu sana, hasa katika uchumi wa viwanda, vipimo vinatakiwa viwe sahihi ili majengo yawe imara kwa ajili ya kukuza uchumi

wetu.

"Wakati mwingine cement (sarufi) inaweza kutoka kiwandani ikiwa sahihi, lakini wafanyabiashara wanapunguza, huko ni kuhujumu uchumi wa nchi," alisema Mavunde.

Alisema pia wamekuwa wakipita viwandani mara kwa mara na kwenye maduka kuwaelimisha wazalishaji na wafanyabiashara kuhusu matumizi ya vipimo katika bidhaa mbalimbali za ujenzi ili wananchi wapate bidhaa kulingana na thamani ya fedha wanazotoa. Mavunde alisema wakala una jukumu la kumlinda mliji katika matumizi ya vipimo sahihi, vinavyotumika kwenye biashara na huduma nyingine.

Alisema Mkoa wa Kinondoni kuna kata 34 zilizopo wilaya za Ubungo na

Kinondoni ambazo wanazifikia zote kwa wakati na kwa mwaka 2019/20 walikadiriwa kuhakiki vipimo 61,626 na hadi kufikia robo ya tatu (Machi 2020) wamehakiki 51,393 sawa na asilimia 83.4 ya lengo.

Mavunde alisema kulingana na Sheria ya Vipimo sura ya 340, ni kosa la jinai kutumia vipimo batili na atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria, ikiwa ni pamoja na kutozwa faini au kufikishwa mahakamani ambako akikutwa na hatia atastabili kifungo, faini au vyote kwa pamoja.

Wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi Mwenge, walipongeza ukaguzi huo na kuomba uendelee kufanyika mara kwa mara ili kuhakikisha mwananchi analindwa ipasavyo katika matumizi ya vipimo.

MWANANCHI UK 19

onywa * TADB yatoa * Sh300 mil kwa wavuvi

kati ya Juni 24 na 25
ena, ili kupitia yote
wa na changamoto

te ambayo yatakuwa
kazi yetu itakuwa ni
hatua, kwani lengo
hakikisha kunakuwa
wa kufanya biashara,"
iziri Kamwelwe.
ema nyaraka nyingi
ikiwa zinapokwen-
wakala wa forodha
muda mwingi, hali
utoaji wa makontena.
moja yenye makon-
inapocheleweshwa
te makontena yote
ra kutoka, tukumbuke
baliano ya kufanya
4 katika siku saba,"

Johari Shani, Mwananchi
mwananchipapers@
mwananchi.co.tz

Buchosa. Benki ya Maende-
leo ya Kilimo (TADB) imetoa
mkopo wa Sh300.7 milioni kwa
vyama vya ushirika vya wavuvi
kwa Wilaya za Sengerema na
Ukerewe mkoani Mwanza.

Vyama hivyo ni Chama cha
Ushirika cha Bukasiga Fisheries
Co-operative Society Ltd, kili-
chopo kijiji cha Kamasi Ukerewe
kilichokabidhiwa Sh200 milioni
na Zilagula cha halamshauri
ya Buchosa kilichokabidhiwa
Sh100.7 milioni.

Akizungumza kwa nyakati
tofauti jana wakati akikabi-
dhi hundi ya fedha hizo, Naibu
Waziri wa Mifugo na Uvuvi,
Abdallah Ulega alisema mkakati
wa Serikali ni kuwainua wavuvi
waweze kuanzisha viwanda
vidogo kupitia benki hiyo.

Ulega alisema wizara itakuwa
msimamizi wa mikopo hiyo na
kuhakikisha wavuvi wanainuka
kupitia shughuli zao.

"Viongozi wa ushirika wek-
eni taarifa zenu vizuri, tuna-
taka viwanda vidogo vidogo vya
wafugaji na wavuvi vikiwemo
vya kukausha dagaa, minofu ya
samaki na kutengeneza kayabo
nzuri, ili mpeleke bidhaa hizo
kwenye masoko ya ndani na nje
ya nchi," alisema Ulega.

Pia, Ulega alisema Serikali
imejipanga kuanzisha kanzi
data (mfumo wa kupokea taar-
ifa za wavuvi kila siku) ili kua-



300m 100m

Jumla ya miko-
po iliyotolewa
na TADB kwa
vyama vya ush-
irika vya wavuvi
Wilaya ya Sen-
gerema

Kiasi cha
mkopo kilicho-
patiwa chama
cha ushirika
Zilagula.

minika na taasisi za kifedha na
kupatiwa mikopo.

Mkurugenzi Mkuu wa TADB,
Japhet Justine alisema kutoa
mikopo hiyo kupitia ushirika
inakuwa rahisi kwa wahusika
kuwa na nidhamu ya fedha wan-
apewa badala ya kumkopesha
mtu mmoja mmoja.

Alisema benki hiyo inatoa
mikopo hiyo ili kuona wafugaji
na wavuvi wengi wananufaika.

Naye Mwenyekiti wa Chama
cha Ushirika Zilagula, Joram
Yuda alisema wanaishuku-
ru Serikali kwa kuwa wavuvi
wameanza kuaminika na taa-
sisi za kifedha kwa kuwa wame-
anza kuaminika kwa kupatiwa
mikopo, ili kujiendeleza katika
sekta hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa Cha-
ma cha Ushirika cha Bukasiga,
Jumbura Lugola alisema hatua
hiyo itakuwa mkombozi kwao
kwa kuwa wamekuwa wakid-
haraulika na taasisi za fedha
kwa madai ya shughuli zao
kutoaminika.

nda

owa wilayani Iramba
ekezaji mzawa, hivyo
ana uwekezaji wake

Serikali na Baraza la
wa Mazingira (NEMC)
eni ya athari za maz-
esababisha kiwanda
elewa uzalishaji.
waka 2015, Meneja wa
na Mount Meru Mill-
a Mwakabuta alisema
hakula cha mchana
unzi ili kuwahamasi-
na sambamba na kui-
usiano.



TVLA partners with EA firm in easing disease in Tanzanian cattle

By Henry Mwangonde

THE Tanzania Veterinary Laboratory Agency (TVLA) has signed a Memorandum of Understanding (MoU) with Breeding East Africa (ABEA) for the supply of Fluorescence Polarization Assay (FPA), a tool used in laboratories to diagnose *Bucella abortus*, an infection which causes reproductive problems in cattle.

Also known as Brucellosis, the viral disease causes problems such as abortions, stillbirth and infertility in most species of animals. Other signs can include arthritis in cows and pigs, mastitis and lameness in goats, and oozing skin lesions in horses.

Speaking during the signing ceremony on Monday, TVLA Chief Executive Officer Dr Furaha Mramba said the tool which is widely used globally for rapid tests releases results within a short period of time hence will help farmers who have been losing their livestock due to the disease.

"This is a boost to us because the tool helps scientists to easily determine samples of a livestock which has ever been immunized or not within a short period of time," she said.

Dr Mramba said this year alone 11,549 cattle samples were taken for tests and out of the number, 1,141 tested positive for the disease saying this was a clear sign that the disease was a threat to the livestock sector development in the country.

According to her, the tools will be distributed to the country's main veterinary laboratories including the central one which is based in Dar es Salaam.

She said already trials on using the device have been conducted for more than a year before resolving to have it used in the country.

The disease is endemic in many

geographical areas. Despite being controlled in a few developed countries, it is still a problem and a major economic burden globally.

Dr Mramba said the tool will rescue farmers who lose a number of their cattle due to the disease because early diagnosis leads to early actions, the tool will help early diagnosis of the deadly disease.

She added that the agency will now conduct tests for farmers at a cost of 2000/- instead of 5000/- charged before having the tools.

For his part the General Manager for (ABEA) Masele Masunga said the company deals with artificial insemination but Brucellosis disease has been the main setback.

"We decided to come up with FPA because currently it takes three to four days to have results of a single test, but at the same time the current testing system only takes blood samples with FPA we can even test milk samples," he said.



This is a boost to us because the tool helps scientists to easily determine samples of a livestock which has ever been immunized or not within a short period of time



Livestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega (C) pictured at the weekend presenting a dummy cheque for a 200m/- Tanzania Agriculture Development Bank loan to members of Ukerewe District's Bukasiga Fishing Cooperative Society. Photo: Correspondent Neema Emmanuel

Agro-bank gives 200m/- loan to fishing group in Ukerewe District

By Guardian Correspondent, Ukerewe

IN order to enable the country to attain middle economy status by 2025 through the industrial sector the Bukasiga Fisherman Association in Ukerewe District in Mwanza Region has been provided with 200m/- loan from the Tanzania Agricultural Bank (TADB).

The money will be used for the construction of ice making factory and equipment for drying sardines both aimed at adding value to fish products.

Speaking during the event to present the cheque to the Association, the Deputy Minister for Livestock and Fisheries Abdallah Ulega said in order to attain that goal, fishermen should work hard as there was no shortcut to development.

He said during its first years, the fifth phase government had placed robust strategies that ensured fishermen are trusted to be given loans from TADB.

"In five years since its establishment, TADB has provided more than 170 billion loans in the agricultural, livestock and fisheries sectors and for the first time since independence fishermen are now being trusted to receive loans and that fish is not a seasonal crop, but perennial," Ulega said.

He thus urged them to be patriotic and trustworthy in managing the funds they have been provided with and advised the Prevention and Combating of Corruption Bureau in the district to advise association members over the need for honesty and not to wait until things start going wrong.

He added: "The government's

strategy is to establish cooperatives for livestock keepers and fishermen and in regard to fishermen the available statistics are fine but when you repay the loans I will be your advocate and persuade the TADB to give you more loans."

TADB Managing Director Japhet Justine said fishing is a very important sector in Lake Victoria as there is an abundance of fish and what is needed is to engage in modern fishing methods, in order to realise President John Magufuli's dreams.

He said the fishermen have succeeded to get the loan after the Livestock and Fisheries Ministry had ensured that the fishing methods would be modern. "We want an ice making factory and equipment for drying the sardines that has the capacity to preserve the fish up to one year... We are doing this to ensure our resources become beneficial as it is the period for competition hence the products' quality is important and TADB will never abandon you," Justine said.

The board chairman of Bukasiga Fisherman Association Erasto Majula said the association has 62 members and own three land plots for their fishing activities.

He said in one plot of one acre they will construct the ice making factory, another one will be for drying sardines, and the third will cater for offices and a shed for 22 houses to be used as fishermen's camp. "Our aim is to increase employment opportunities for our youth and women, add value to fish products and enhance their preservation capacity," Majula added.

LSU-preservation capacity: Majumda added.

'Pemba salt penetrates world markets'

By Guardian Reporter, Zanzibar

ZANZIBAR Minister for Trade and Industry Amb Amina Salum Ali has said salt produced in Pemba has proved famous and attained great success in the markets of Europe and Canada.

Speaking in the Zanzibar House of Representative, Amb Amina said that is good news for salt production dealers from Pemba in displaying their creativity at dressing up the product.

She said the salt that contains iodine has penetrated into the world market after it has been dressed up by adding various spices.

"I like to inform members of the House that already salt production in Pemba Island by Swahili Coast Salts has attained great success by penetrating into the European market," she said.

She lauded the creativity by Swahili

Said for displaying the capability in producing quality salt that has penetrated into the competitive world market.

She said her ministry's strategies are to strengthen the industrial investment sector from entrepreneurial to big industries in order to add to the GDP.

She said there are a total of seven industries established by indigenous entrepreneurs in the period of 2019-20 producing various products that have

entered the market.

"The Zanzibar government congratulates indigenous investors in the small industry sector which have also assisted in job creation," she said.

She said the government has allocated a total of 6.85bn/- through the Zanzibar Small and Medium Industry Development Agency (SMIDA) for industrial and entrepreneurial development.

developmental stage of the child

* Mawaziri, makatibu wakuu wajadili biashara ya samaki

Na Judith Ferdinand,
Mwanza

■ ■ ■ ILI kuhakikisha biashara ya minofu ya samaki katika masoko ya nje ya nchi inakuwa endelevu, mawaziri wa wizara tatu, makatibu wakuu pamoja na wakuu wa Mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara wamekutana kwa ajili ya kuweka mikakati ya pamoja ya biashara ya samaki kwenda nje ya nchi.

Kikao hicho kilichofanyika jana mkoani Mwanza na kuhudhuriwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isacka Kamwelwe, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Luhaga Mpina, Waziri wa Viwanda na Biashara Innocent Bashungwa, Makatibu Wakuu wa Wizara husika akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Rashid Tamatamah.

Akizungumza wakati akifungua kikao hicho Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isacka Kamwelwe, alisema lengo la kikao hicho ni kuweka mikakati ya pamoja itakayoweza biashara iliyoanza Mei 12, mwaka huu ya kusafirisha samaki kwenye masoko ya nje kutokea Uwanja wa Ndege

wa Mwanza inakuwa endelevu. Kamwelwe alisema mpango huo utawezesha kukuza uchumi wa wananchi wa Kanda ya Ziwa pamoja na taifa kwa ujumla.

Alisema wananchi watapata faida moja kwa moja katika mnyororo huo wa biashara pamoja na wazalishaji wa samaki na taasisi ambazo zitakusanya tozo kutokana na huduma zitakazotolewa.

Alisema taasisi hizo ni pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Mamlaka ya Udhidhiti Usafiri wa Anga na Mamlaka ya Hali ya Hewa na kwamba pale itakapoweza kwa waongeze aina zingine za bidhaa au mazao yanayoweza kusafirishwa kwenda masoko ya nje ya nchi ili kuongeza wigo wa wanufaika kama vile wanavyojua kuwa ukanda huu ni wa mifugo ikiwemo ng'ombe na mbuzi.

"Kwa maelekezo hayo, niliagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi akutane na wenzake wa Mifugo na Uvuvi pamoja na wa Viwanda na Biashara ili wafanye uchambuzi na kushauri namna bora ya kushirikiana katika maeneo yanayotuhusu na kuifanya biashara ya usafirishaji minofu ya

samaki kutokea katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza iwe endelevu pamoja na kuhakikisha tunakuwa na ndege yetu ya mizigo ambayo itabeba mizigo/minofu ya samaki ya kudumu na uhakika," alisema Kamwelwe.

Aidha alitumia fursa hiyo kueleza kuwa tangu kuanza kwa safari za kubeba samaki kutoka Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwenda masoko ya Ulaya kumekuwa na jumla ya safari nne ambapo kati ya hizo tatu zilikuwa za Shirika la Ndege la Rwanda na moja ya Shirika la Ndege la Ethiopia.

Hata hivyo alisema katika safari hizo kumejitokeza changamoto mbalimbali zilizowasilishwa na mashirika hayo ya ndege kupitia maafisa wao wa masoko pamoja na kuwepo hoja mbalimbali zinazohitaji kutafutiwa ufumbuzi zilizowasilishwa na wazalishaji wa samaki.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tamatamah, alisema Serikali imeanzisha mchakato wa kusafirisha minofu ya samaki moja kwa moja kutoka mkoani Mwanza hadi nje ya nchi, hivyo wasingependa uishie

katikati ndio maana wameamua kuwa na kikao hicho baada ya changamoto ambazo zimejitokeza na zisipotatuliwa zinaweza kufanya mashirika ya ndege yanayokuja kuchukua samaki yasishe safari.

"Kila wizara tumegawana majikumu mbalimbali katika kutatua hizo changamoto zilizojitokeza katika kikao cha pili kitakachofanyika Dodoma kila wizara inapaswa kuleta mrejesho wa wapi walipofikia katika kutatua changamoto hizo, wizara yetu kwa muda wa miaka miwili iliopita viwanda vingi vilisimamisha uzalishaji. Lakini sisi kwenye Wizara yetu mchakato ambao tumeufanya ni operesheni ambayo baada ya miaka miwili imezaa matunda, sasa hivi samaki wameongezeka kiasi kwamba viwanda vinafanya uzalishaji kwa kiasi kikubwa ambapo changamoto kubwa kwa sasa ni masoko," alisema.

Alisema mwaka jana walianza mchakato wa kuhamasisha wachakataji wadogo kuanzisha vikundi na kugandisha samaki na kuzaa sehemu mbalimbali nchini.

Pia aliwataka watu wa Kanda ya Ziwa kuacha kutumia zana haramu na badala yake wajikite katika kutafuta masoko.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, akisisitiza jambo katika kikao cha kujadili mkakati wa pamoja wa kuhakikisha usafirishaji samaki unaendelea na kuwa na manufaa kwa wananchi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa, jana. (Picha na Judith Ferdinand)

Ministers, RCs call for sustainable export markets for Tanzania fish

By Guardian Correspondent, Mwanza

CABINET ministers and regional commissioners from the Lake Zone regions yesterday met to formulate a joint strategy to ensure foreign market sustainability for the fish fillet trade.

The meeting convened in Mwanza was attended by the Minister for Works, Transport and Communications Isack Kamwelwe, the Minister for Livestock and Fisheries Luhaga Mpina and the Minister for Industry and Trade Innocent Bashungwa, their Permanent Secretaries including the Permanent Secretary to the Ministry for Livestock and fisheries Rashid Tamatah, and Regional Commissioner from Mwanza, Kagera and Mara regions.

Speaking when opening the meeting, Works transport and communications minister Isack Kamwelwe said the aim of the meeting was to draw a joint strategy that would sustain the fish fillet export trade that began May 12 this year.

He said the plan will inspire economic growth for the people of the Lake Zone and the nation in general as those who will directly benefit from the whole chain of the trade are the fishermen

Permanent Secretary to discuss with his counterparts to assess and advise on how to cooperate in areas involved to make the fish fillet export trade from Mwanza airport sustainable," Kamwelwe said.

He also used the occasion to explain that since the fish fillet export trade began, four plane had transported the product from Mwanza Airport, out of which three were by RwandAir and one by Ethiopian Airline.

He said the trips raised various challenges that were submitted by the airlines through their marketing officers, of which solutions thereof had to be found.

The PS to the Ministry of Livestock and Fisheries, Rashid Tamatamah said since the government started the fillet export trade, it would not augur well to stop midway hence solutions had to be found on the challenges raised in order that airlines do not suspend services to airlift the fish fillet to European markets.

He said the work done by his ministry had borne fruit after two years as now the production of fish fillets had increased as the factories thereof are